UWAZI WA DALILI

JUU YA UHALALI WA DALALI NA YALE YANAYOFUNGAMANA NA MADALALI

MTUNZI

ABUU MUHAMMAD HASNUU AMOUR KOMBO

AZIINJIBARY ATTANZANIY

مكتبة الإمام الأوزاعي بن جبير

UWAZI WA DALILI JUU YA UHALALI WA UDALALI NA YALE YANAYOFUNGAMANA NA MADALALI

MTUNZI

ABUU MUHAMMAD HASNUU AMOUR KOMBO

AZZINJIBARY ATTANZANIY

Kitabu hichi ni haki ya mmiliki (muandishi) na si ruhusa kutowa kopi isipokua kwa ruhusa ya mwenye kitabu.

(m) Abuu Muhammad Hasnuu Amour

Kimeandikwa kitabu hichi tarehe 16/12/2022 na kuchapishwa na kutolewa tarehe 1/4/2023 na kimechapishwa Maktabatul Imamil Auzaai'y Zanzibar.

مكتبة الإمام الأوزاعي بن جبار

MAKTABATUL IMAMIL AUZAAI'Y
ZANZIBAR TANZANIA
0779819880 0772719464
0776959197

بسم الله الرحمن الرحيم

UTANGULIZI

Kila sifa nyema na shukrani zote anastahiki kusifiwa na kushukuriwa Allah (Subhaanahu Wataala) ambaye aliyemfundisha mwanaadam yale aliyokuwa hayafahamu kwa msaada wa kalamu na kumuondoshea ujinga na kumuweka kwenye nuru ya elimu.

Swala na salamu ziwe juu ya kipenzi chetu Bwana Mtume (Salallahu Alayhi Wasallam) ambaye ametumwa kujawafikishia viumbe wa Allah (Binaadamu na Majini) nuru ya elimu itokayo kwa Mola wao Mlezi.

Amma baada ya shukrani hizo na kumtakia swala na salamu kipenzi chetu na Mteule wa umma huu naye si mwengine isipokuwa ni Bwana Mtume (Salallahu Alayhi Wasallam). Uislamu umemtaka mja kila jambo lake alifanye kwa misingi ya elimu na kujiweka mbali na ujinga, kwa ajili hiyo basi tumeonelea na kutilia umuhimu kuandika kitabu hichi ambacho kitakuwa ni msaada mkubwa kwa wale ambao wanaojishughulisha na kazi za udalali na yale yanayofungamana nayo kwa mujibu wa sheria ya kiislamu.

Na kitabu hichi tumekiita na kukipa jina: **“UWAZI WA DALILI JUU YA UHALALI WA UDALALI NA YALE YANAYOFUNGAMANA NA MADALALI”**.

Kwa kuweka kitabu hichi na kukiandika kwake itakuwa ni mwangaza kwa wale ambao wanaofanya kazi hii na itakuwa ni wepesi kwao na ni rahisi kuifanya kazi yao hii kwa misingi ya elimu na kuchunga mipaka ya uislamu na pia kitabu hichi kitawaondoshea shaka juu ya uhalali wa kazi hiyo.

Tunamuomba Allah (Subhaanahu Wataala) kwa majina yake matukufu na sifa zake nyema ajaaliye kitabu hichi kiwanufaishe waislamu wote na kiwe ni kwa ajili yake na kiwe ni katika mizani ya mema yetu siku ya kukutana na yeye, siku ambayo haitomnufaisha mtu mali yake wala watoto wake isipokuwa matendo yake mema aliyofanya kwa ajili ya Allah (Subhaanahu Wataala)

Aaaamii

Abuu Muhammad Hasnuu Amour Kombo

Azzinjibariy Attanzaniy

MAANA YA UDALALI

Maana ya udalali: Ni kukaa kati na kati baina ya muuzaji wa bidhaa na mnunuzi wa bidhaa.

Maana ya Dalali: Ni yule mtu ambaye hukaa na kuingia kati na kati baina ya muuzaji wa bidhaa au mmiliki wa bidhaa na baina ya mnunuzi wa bidhaa, na huyu Dalali ameitwa kwa jina la Dalali ni kwa sababu yeye ndiye anayemjuulisha mnunuzi wa bidhaa wapi ilipo bidhaa nzuri na inayohitajika na pia kumjuulisha muuzaji wa bidhaa juu ya thamani ya bidhaa anayokusudia kuuza.

UMUHIMU WA KUWEPO UDALALI

Kuwepo kwa udalali baadhi ya wakati kuna umuhimu mkubwa na kunapatikana faida kubwa na haya ni kama waliyoelezea wanachuoni

والسمسر يحتاج الناس إليها كثيرًا، فكثير من الناس لا يعرفون طرق المساومة في البيع والشراء، وآخرون ليس عندهم قدرة على تمحيص ما يشترون ومعرفة عيوبه، وآخرون ليس عندهم وقت لمباشره البيع والشراء بأنفسهم. ومن هنا كانت السمسرة عملا نافعا، ينتفع به البائع والمشتري والسمسار.

“ Na udalai ni jambo ambalo watu wanalihitajia kwa wingi (kwa sanna), basi wengi katika watu hawatambui na kujua njia za mapatano katika biashara baina ya Muuzaji na Mnunuzi katika kuuza na kununua, na watu wengine hakuna kwao uwezo juu ya kutambua na kujua usafi na uzuri wa kile wanachokinunuwa na kujua ni zipi aibu zake, na watu wengine hakuna kwao wakati wa kuingia katika mauziano na manunuzi ya kibiashara. Na kutokana na maelezo haya hapa, imekuwa udalali ni kazi yenye manufaa, hunufaika nayo kazi hiyo Muuzaji na Mnunuzi na Dalali mwenyewe”.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): “ Manufaa ya kazi ya Udalali yatapatikana ikiwa pande zote zimechunga masharti ya kazi hii, masharti ambayo yamewekwa na sharia ya Uislamu na pande zote hizo zikachunga masharti hayo, Muuzaji, Mnunuzi na Dalali mwenyewe na kukosekana dhulma baina yao na kila mmoja kumuhurumia mwengine”.

MASHARTI YA KAZI YA UDALALI

Ili kazi ya udalali iwe ni sahihi ni vyema kuchungwa masharti haya yafuatayo:-

1. Pachungwe uadilifu na ukweli baina ya pande zote tatu, upande wa mmiliki wa mali, upande wa mnunuzi, na upande wa Dalali.

2. Kupatikana mawafikiano na muwafaka pamoja na maridhiano baina ya Dalali na ule upande ambao Dalali atachukua ujira wake juu ya kazi yake hii ya udalali kabla ya kuikamilisha kazi, na hili linakuwa kwa yeye dalali kutolea maelezo kuwa kwa mujibu wa kazi yake atachukuwa kiwango fulani cha mali baada ya kuuzwa kwa mali yote kwa kule kusimamia kwake zoezi zima la kuuzwa kitu husika, basi mmiliki wa mali akikubali hilo, hapo Dalali atatumia juhudi yake ya kutafuta wateja na kusimamia kuuza kwake mali hiyo.

TANBIHI: Baadhi ya wakati mmiliki wa mali ndie anaetoa maelekezo ya kuwa yeye mali yake anataka iuzwe kwa bei maalumu ambayo huiainisha na kusema kuwa atampa dalali ujira wake (malipo yake) kwa kazi yake ya kutafuta wateja na kusimamia kuuzwa kwa kitu husika au mali husika na kumtajia kiwango maalum, hili pia hukubalika ikiwa yamepita maridhiano baina ya pande zote mbili, au kitakachozidi ni cha dalali pia hili hukubalika.

3. Baadhi ya wanachuoni wamesema: Kuwa huo udalali ni lazima ndani yake kuwe kumekusanywa na taabu na mashaka ya ufatiliaji wa mauziano na kukamilika kwake.

4. Panaekewa sharti pia Dalali anatakiwa awe ni mjuzi wa kuzijua bidhaa zilizo kuwa ni nzuri na zile zilizokuwa siyo nzuri ili kujua kwake huko kutamfanya awe ni mwenye kuchunga uhalali wa kile anachokisimamia.

5. Dalali ajitahidi kujiepusha na kufanya khiana katika kazi yake hii ya udalali kwani khiana ni jambo lililokatazwa katika kila hali na dalili ya hayo ni maneno ya Mtume (Salallahu Alayhi Wasallam) :

وعن أبي هريرة رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قال: قال رسول الله صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: « مَنْ حَمَلَ عَلَيْنَا السِّلاَحَ فَلَيْسَ مِنَّا، وَمَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا ». رواه مسلم (١٠١) وفي رواية أخرى: « مَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا، والمكرُ والخداع في النار ».

Na kutoka kwa Abuu Hurayra (Radhiyallahu Anhu) Amesema: Amesema mjumbe wa Allah (Salallahu Alayhi Wasallam): “ Yoyote atakaebeba silaha dhidi yetu si katika sisi, na yoyote atakaetufanyia khiana na khushi si katika sisi ”. Na katika riwaya nyengine : “ yoyote atakaetufanyia khiana si katika sisi, na mwenye kufanya vitimbi na mwenye kufanya khadaa ni watu wa motoni ”.

6. Dalali ajiepushe na kuleta madhara baina ya pande mbili, baina ya mmiliki wa mali na mnunuzi wa mali katika mauziano na manunuzi yao na dalili ya hayo ni maneno ya Mtume wetu kipenzi yanayosema :

وعن عبادة بن صامت رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، قال النبي ﷺ: « لَا ضَرَرَ وَلَا ضِرَارَ » رواه ابن ماجه (١٩٠٩) وصححه الألباني في ((صحيح ابن ماجه)).

Na kutoka kwa Ubaadata bin Swaamit (Radhiyallahu anhu) Amesema Mtume (Salallahu Alayhi Wasallam) : “ Hakuna kufanya madhara na hakuna kulipiza madhara ”. au kwa maana nyengine: “ Haifai kufanya madhara bila ya kukusudia na wala haifai kufanya madhara kwa kukusudia ”.

7. Dalali anatakikana awe muaminifu na achunge amana atakayokabidhiwa, kama katika bidhaa kutakuwa na aibu ni vyema kuweka wazi ili ijulikane kabla ya mauziano kupita ili atakaenunuwa bidhaa hiyo awe anajua kabla na iwe ni wepesi kwake kuchukuwa maamuzi yaliyo sahihi katika kununua bidhaa hiyo

8. Dalali atakapobainikiwa kuwa Mmiliki wa mali, bidhaa anayotaka itafutiwe mteja na kuuzwa ni bidhaa ya haramu, basi dalali anatakikana ajiepushe na kuliingia jambo hilo na awe mbali nalo kwani bidhaa yake ipo katika misingi ya haramu na wala asifanye tamaa kwa kuliingia jambo hilo kufanya hivyo ni kuisaidia haramu iwe na nguvu na Allah (Subhaanahu Wataala) Anasema katika Suratul Maida aya 2:

﴿ وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ وَلَا تَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡإِثۡمِ وَٱلۡعُدۡوَٰنِۚ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلۡعِقَابِ ٢ ﴾ [المَائِدَة : ٢]

“ Na Saidianeni juu ya wema na taqwa (Uchaji) na wala musisaidiane juu ya madhambi na kufanya uadui, na muogopeni Allah, hakika Allah ni mkali wa kuadhibu ”.

DALILI ZINAZOJUULISHA JUU YA UHALALI WA KAZI YA UDALALI

Miongoni mwa dalili zilizokuja kuhusiana na udalali ni hizi zifuatazo:-

١- وَعَنْ قَيْس بن أَبي غَرَزَة رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: " كُنَّا بِالمَدِيْنَةِ نَبِيْعُ الأَوْسَاقَ وَنَبْتَاعَهَا، وَكُنَّا نُسَمِّي أَنْفُسَنَا السَّمَاسِرَةَ، وَيُسَمِّيْنَا النَّاسُ ، فَخَرَجَ إِلَيْنَا رَسُوْلُ اللهِ ﷺ ذَاتَ يَوْمٍ، فَسَمَّانَا بِاسْمٍ هُوَ خَيْرٌ مِنَ الَّذِيْ سَمَّيْنَا أَنْفُسَنَا، وَسَمَّانَا النَّاسُ، فَقَالَ: « يَا مَعْشَرَ التُّجَّار إِنَّهُ يَشْهَدُ بَيْعَكُمْ الصلفُ الكَذِب فشُوبوه بالصدقة » . أ خرجه أبو داود (٣٣٢٦) والنسائي (٣٨٠٠) والترمذي (١٢٠٨) وغيرهم وصححه الألباني في ((صحيح النسائي)) (٣٨٠٩) وفي غيره من كتيه رَحِمَهُ اللَّهُ تعالى.

1- Na kutoka kwa Qais bin Abiy Gharaza (Radhiyallahu Anhu) amesema: “ Tulikuwa sisi katika mji wa Madina tukiuza na kununua bidhaa kwa vipimo vya wasqi, na tulikuwa tukijiita madalali sisi wenyewe na watu walikuwa wakituita hivyo, basi akatoka Mtume (Salallahu Alayhi wasallam) kutujia sisi siku moja, basi na akatuita kwa jina hilokuwa zuri zaidi kuliko lile jina ambalo tulilokuwa tukijiita sisi wenyewe na watu wakituita kwa jina hilo, basi Akasema: Enyi kundi la wafanya biashara, hakika biashara zenu (kuuza na kununuwa kwenu) zinahudhuriwa na viapo na uongo, basi zichanganyeni hizo biashara zenu na kutoa sadaka”.

Makusudio ya ndani: Wafanya biashara wengi huwa wanaapa na kusema uongo wakiwemo madalali pia kwa hiyo pale panapotokea jambo hilo

kwenye biashara kuweni na kawaida ya kutoa sadaka kwani sadaka husafisha vitu hivyo.

Wanasema Wanachuoni wa hadithi kama ifuatavyo:-

" وفي حديث قيس بن أبي غرزة أنّ السمسرة مشروعة وجائزة "

“ Na ndani ya hadithi ya Qais bin Abiy Gharaza hakika jambo la udalali ni lenye kuekewa sheria na ni jambo linalofaa ”.

٢- وعن أبي هريرة رضي الله عنه قال: قال رسول الله ﷺ : « المُسْلِمُوْنَ عَلَى شُرُوْطِهِم » الحديث. أ خرجه أبو داود (**٣٥٩٤**) وغيره وصححه الألباني في ((صحيح أبي داود)) وقال: ((حسن صحيح)).

2- Na kutoka kwa Abuu Hurayra (Radhiyallahu Anhu) Amesema: Amesema Mtume wa Allah (Salallahu Alayhi Wasallamu): "Waislamu wapo juu ya sharti zao walizokubaliana”.

Wanachuoni wanasema wakati walipokuwa wakitolea maelezo hadithi hii kama ifuatavyo:-

" أي: ثابتون على الشروط الجائزة شرعًا التي تقع بينهم ؛ فيوفون بها ولا يرجعون عنها؛ لأن هذا من الوفاء بالعقود الذي أمر الله به، وأما الشروط الفاسدة أو غير الجائزة شرعًا؛ فلا يوفى بها " .

“ Maana yake: Ni (Waislamu) wenye kuthibiti juu ya sheria zilizokuwa ni zenye kufaa kisheria ambazo hutokezea baina yao (au kwa yale

yanayotokea baina yao), basi hutekeleza (mambo yao) kwa sheria hizo na wala hawarejei nyuma wakaziacha sheria hizo kwa sababu kufanya hivi ni katika kutekeleza vifungo au ahadi ambazo Allah ameziamrisha, na amma sharti zilizokuwa ovu au mbaya (zinazokwenda kinyume na sheria ya uislamu) au zilizokuwa hazifai kisheria, basi hazitotekelezwa sharti hizo".

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): " Udalali ni mafungamano ya mkataba imma baina ya mmiliki wa mali na Dalali au mnunuzi wa bidhaa na Dalali, na mkataba huo hufungwa kwa masharti na sheria ambazo hukubaliana baina yao kwa hiyo ni vyema kila mmoja kuchunga masharti hayo na sheria hizo na kutofanya khiana kwa mwenzake".

٣- وقال ابن عباس رضي الله عنهما: ((لا بأس أن يقول: بع هذا الثوب، فما زاد على كذا وكذا فهو لك)). أورده البخاري في ((صحيحة)).

3- Na amesema Ibnul-Abbas (Radhiyallah Anhuma): " Hakuna ubaya kusema: Uza nguo hii, na kitakachozidi juu ya kadha wakadhaa (Zaidi ya hapo) basi hicho ni chako ".

٤- وقال ابن سيرين: ((لَا بَأْسَ بِأَجْرِ السمسار إذا اشترى يدًا ببيدٍ)). وقال أيضًا: ((إِذَا قَالَ: بِعْهُ بِكَذَا، فَمَا كَانَ مِنْ رِبْحٍ فَهُوَ لَكَ، أَوْ بَيْنِي وَبَيْنَكَ، فَلاَ بَأْسَ به)). أورده أيضًا البخاري في ((صحيحة)) في كتاب الإجارة.

4- Na amesema Ibnu Siriina: " Hakuna ubaya kwa ujira (malipo) wa Dalali (kwa kazi yake) wakati atakaponunua mkono wa mkono ". Na akasema tena vile vile: " Atakaposema (mwenye mali au mmiliki wa mali): Uza hiyo mali (bidhaa) kwa bei kadhaa, na kitakachokuwa katika faida basi hicho ni chako, au ni baina yangu na baina yako (tugawane), basi hakuna ubaya kwa hilo "

٥- وسئل عطاء عن السمسرة فقال: " لَا بَأْسَ بِهِ ".

5- Na alipoulizwa Atwaau kuhusiana na udalali na akajibu kwa kusema: “ Hakuna ubaya kwenye udalali ”.

Amesema Imam Hafidh Ibnu Hajar wakati alipokuwa akitolea maelezo juu ya athari hizi ambazo amezileta Imam Bukhari ndani ya sahihi yake, kwa kauli yake hii ifuatayo:-

" وكأن المصنف أشار إلى الرد على من كرهها "

“Na kama kwamba mtunzi wa kitabu (Imamu Bukhari) ameashiria kuwapinga na kuwaradi wale ambao wanaochukia jambo la udalal ”

Maelezo ya Ziada: Jambo hili la udalali sheria imeliruhusu na ni jambo jema na kipato kitakachopatikana ni kipato cha halali, lakini kwa kuchungwa masharti yaliyotangulia na pia kupatikana uwazi na ukweli ndani ya kazi hii.

KAULI ZA WANACHUONI JUU YA KAZI YA UDALALI NA UHALALI WAKE

Kipengele hichi ni muhimu sana kwani dalili zinazokuja zikawa zinazungumzia jambo fulani ili dalili hizo zifahamike vizuri na kwa uwazi ni vyema kuwarejea wanachuoni na hapa napenda kunukuu baadhi ya kauli za wanachuoni juu ya uhalali wa kazi hii ya udalali, nazo ni kama zifuatazo:-

١- قال البخاري رَحِمَهُ اللَّهُ تعالى في ((صحيحه)): " باب أجر السمسرة. ولم ير ابن سرين وعطاء وإبراهيم والحسن بأجر السمسار بأسًا ".

1- Amesema Imam Bukhariy (Rahimahullahu): “ Mlango unaozungumzia ujira (malipo) wa Udalali, na hakuona Ibnu Siriina na Atwaao na Ibrahim na Hassan kwa ujira wa Dalali hawajaona kuwa kuna ubaya wowote ule ”.

٢- وسئل الإمام مالك كما في ((المدينة)) (٣/ ٤٣٣) عن أجر السمسار فقال: " لا بأس بذلك ".

2- Na aliulizwa Imamu Maalik (Rahimahullahu) kuhusiana na ujira (malipo) wa Dalali, basi akajibu kwa kusema: “hakuna ubaya katika ujira wa Dalali”.

٣- وقال ابن قدامة رحمه الله تعالى في ((المغني)) (٥/ ٨٢): " إذا قال: بع هذا الثوب بعشرة فما زاد عليها فهو لك صح، واستحق الزيادة، وقال الشافعي: لا يصح، ويدل لصحة هذا: أن ابن عباس كان لا يرى بذلك بأسا، ولأنه يتصرف في ماله بإذنه، فصح شرط الربح له ... "

3- Na Amesema Ibnu Qudaamah (Rahimahullahu): “ Atakaposema (Mmiliki wa mali au bidhaa): Uza nguo hii kwa kumi (Dinari, Dirham, Riyali n.k), basi itakachozidi juu yake basi hicho ni chako, itafaa na kusihi (jambo hilo) na itastahiki ziada kwa Dalali, na Amesema Imamu Shafi (Rahimahullahu): “ haitosihi ” na kinachojuulisha kusihi kwa jambo hili (la udalali) hakika Ibnu Abbasi alikuwa haoni ubaya kwenye jambo hilo (la udalali), na kwa sababu yeye (Dalali) anaitumia mali yake na kuishughulikia kwa idhini yake (yaani Mmiliki wa Mali), basi inasihi na kufaa sharti ya kupata faida kwa ajili yake”.

٤- وقالت اللّجنة الدائمة في ((فتاوى اللجنة الدائمة)) (١٣/ ١٢٩): " إذا حصل اتفاق بين الدلال والبائع والمشتري على أن يأخذ من المشتري، أو من البائع، أو منهما معا، سعيا معلوما جاز ذلك، ولا تحديد للسعي بنسبة معينة، بل ما حصل عليه الاتفاق والتراضي ممن يدفع السعي جاز. لكن ينبغي أن يكون في حدود ماجرت به

العادة بين الناس، مما يحصل به نفع الدلال، في مقابل ما بذله من وساطة وجهد لإتمام البيع بين البائع والمشتري بزيادته فوق المعتاد".

4- Na Imesema Lajnat-Ddaaimah (Jopo la wanachuoni nchini Saudia Arabia): “ Patakapopatikana makubaliano baina ya Dalali na Muuzaji na Mnunuzi juu ya kuchukua Dalali kutoka kwa Mnunuzi au kutoka kwa muuzaji au kutoka kwa wote wawili pamoja, kuchukua mali iliyoendewa mbio na kufanyiwa bidi kuchukua kiwango maalum, inajuzu hilo, na wala hakuna mpaka maalum uliyowekwa katika kuchukuwa mali hiyo iliyofanyiwa bidii na kuendewa mbio kwa mnasaba maalum, bali ni kwa yale yaliyopatikana juu yake makubaliano na maridhiano kutoka kwa yule ambaye ametoa bidii (mpaka bidhaa ikauzwa na kununuliwa) itafaa.

Lakini inatakikana kuwa ndani ya mipaka ambayo imepita kwa jambo hilo desturi baina ya watu, katika yale yanayopatikana manufaa yake kwa Dalali katika usawa wa ile juhudi aliyoitumia katika kukaa kati na kutumia juhudi ya kutimiza mauziano baina ya muuzaji na mnunuzi na wala isiwe ndani yake (ndani ya Udalali) madhara juu ya muuzaji au mnunuzi kwa kuzidisha kwake Zaidi ya kawaida iliyozoeleka”.

FAIDA: Dalali aliyekuwa bora ni yule ambaye anayewaondoshea dhiki watu anaoamiliana nao katika kazi yake ya udalali pamoja na kuwahurumia, na dalili ya haya ni kauli yake Bwana Mtume (Salallahu Alayhi Wasallamu):-

عَنْ جَابِرِ بن عبد الله رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قال: قال رسول الله ﷺ: « رَحِمَ اللهُ رَجُلاً سَمْحًا إِذَا بَاعَ، وَإِذَا اشْتَرَى، وَإِذَا اقْتَضَى ». أخرجه البخاري (٢٠٧٦) وغيره.

Kutoka kwa Jabir Bin Abdillah (Radhiyallahu Anhu) Amesema: Amesema Mtume wa Allah (Salallahu Alayhi Wasallam): “ Allah amrehemu (ammiminie rehma zake) mtu ambaye aliyekuwa na sifa ya upole na kuwafanyia watu wepesi wakati anapouza, na

wakati anaponunuwa, na wakati anapodai madeni yake kutoka kwa masikini”.

Kwa hiyo dalali anaekuwa mpole na kuwafanyia wepesi wale anaoamiliana nao katika mauziano ya bidhaa, huwa anaingia katika orodha ya wale waliyoombewa dua na Mtume wetu kipenzi (Salallahu alayhi Wasallamu).

٥- وأجازه السيد سابق في كتابه ((فقه السنة)) (٨١٨) واحتج بما أورده البجاري في ((صحيحه)) وتقدم ذكره.

5- Na Amelijuzisha jambo la Udalali Assayyid Saabiq katika kitabu chake (Fiq-hu Sunna) (818) na akatolea hoja kwa yale aliyoyaleta Imamu Bukhariy katika sahihi yake na utajo wake umeshatangulia.

٦- وقال ابن باز رحمه الله تعالى: " لا حرج في ذلك (يعني في سمسرة)، السمسار الدلال كونه يبيع له إبله أو بقره أو غنمه أو ثمرته أو ملابس أو ... ، لا حرج، أو أرض أو غير ذلك، يسمى الدلال، لا جرح وهو السمسار".

6- Na Amesema Shekhe Ibnu Baazi (Rahimahullahu): “ hakuna ubaya katika hilo (yaani katika uhalali wa udalali) Dalali ni yule anaekuwa anamuuzia mtu ngamia wake au ng`ombe wake au mbuzi wake au matunda yake, au mavazi yake (nguo zake), au … hakuna ubaya au ardhi au vyenginevyo visivyokuwa hivyo, (huyu) huitwa dalali, hakuna ubaya na yeye ndiye Dalali.”

٧- وقال الشيخ ابن العثيمين رحمه الله تعالى: " يجوز لهذا الذي كان وسيطا أن يأخذ من المال كقدر أجرته، ولكن إن كان اشترط على من كان وسيطا بينهم، فالأمر

واضح، وإن لم يشترط، فإن كان هذا الرجل قد نصبه نفسه لهذه مهنة، استحق الأجر، وإن لم يكن نصب نفسه، فإن عمله هذا يكون تبرعا، لأن من كان بينهم وسيطا، لا يهمون منه إلا التبرع، فإن كان هذا معروفا بأنه الدلال يأخذ الأجر فله الأجر مثله ... ".

7- Na amesema Shekhe Ibnu Uthaimini (Rahimahullahu): “ Inajuzu kwa huyu ambaye amekuwa ni wa katikati (muunganishaji baina muuzaji na mnunuzi) kuchukua kutoka katika mali kama ni kiwango cha ujira wake, na lakini ikiwa ameweka sharti na kupatikana sharti juu ya yule muunganishaji au aliyekaa katikati baina yao, basi jambo lipo wazi, na ikiwa hapajawekwa sharti, basi ikiwa huyu mtu ameiweka nafsi yake na kuisimamisha nafsi yake kwa ajili ya kazi hii (Akaifanya kuwa ndio kazi yake) atastahiki kupata ujira (malipo ya kazi hiyo), na ikiwa hajaifanya hiyo kuwa ndio kazi yake kwenye nafsi yake, basi kwa hakika kitendo chake hichi kitakuwa msaada usiyohitaji malipo, kwa sababu yule aliyekuwa muunganishaji baina yao, wao hawatilii umuhimu jambo lake kutoka kwake isipokuwa ni msaada usiyohitaji malipo, Basi ikiwa huyu (mtu) ni maarufu kwa kuwa yeye ni Dalali anachukuwa ujira (malipo), basi atakuwa na ujira (malipo) mfano wake …”.

٨- وقال الشيخ فوزان حفظه الله تعالى: " هذا يسأل عن السمسار الذي يكون بين البائع والمشتري ويأخذ أجرة؟ نعم لا بأس، يكون الإنسان سمسارا بين البائع والمشتري يسعى بينهما ويكون له أجرة على عمله وسعيه لا مانع من ذلك، لأن هذا مصلح للجميع ".

8- Na amesema Shekhe Fauzani (hafidhahullahu): Huyu anauliza kuhusiana na Dalali ambaye anakuwa baina ya muuzaji na

mnunuzi na akawa anachukuwa ujira (malipo)? Naam hakuna ubaya, mwanadamu kuwa ni Dalali baina ya muuzaji na mnunuzi na akawa anafanya bidii baina yao (ili kuhakikisha mauziano yanakamilika) na inakuwa kwake ujira (malipo) juu ya kazi yake na bidii yake hiyo, hakuna kizuizi (katazo) kinachozuiya jambo hilo, kwa hakika katika jambo hili kuna mashaka kwa wote” [(1)] .

٩- قال أبو عبد الرحمن العزازي في ((تمام المنة)) (٣/ ٣٣٣): " المقصود بالسمسار هو الذي يتوسط بين البائع والمشتري نظير أجر معين، فهذا جائز مباح".

9- Na amesema Abuu Abdi-Rahmaan Al-Azaaziy ndani ya kitabu chake (Tamaamul – Minna, 3/333): “ Makusudio ya Dalali ni yule anaekaa kati na kati baina ya muuzaji na mnunuzi kwa mtazamo wa ujira (malipo) maalumu, basi hili ni jambo linalofaa na ni halali”.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): “ kauli za wanachuoni juu ya mas-ala ya dalali na udalali zipo nyingi sana ila sisi tumefupilizika na hizi tulizozitaja hapa, hii yote inaonesha wazi na kujuulisha kuwa jambo la udalali ni jambo ambalo limeruhusiwa kisheria ila wengi katika madalali wanaoifanya kazi hii ya udalali hawana elimu nayo kazi hii, bali wao wanafanya kimazoea tu na kutochunga sheria zake na vidhibiti vyake, na yoyote ambaye atakaekosea njia na akaacha utaratibu uliyowekwa atapotea tu

" وكل من أخطأ الطريق ضلّ "

“ Na kila mwenye kukosea njia hupotea”.

---

(1) Fatawa za mashekhe: Ibnu Baazi, Ibnu Uthaimin na Fauzani zote zipo kwenye rikodi za kaseti.

HOJA TATA ZILIZOKUJA KUHUSIANA NA UDALALI NA JAWABU ZAKE

Miongoni mwa hoja tata ambazo huwatatiza baadhi ya waislamu katika masala haya ya udalali ni hizi zifuatazo:-

1- Baadhi ya watu husem: “ Udalali ni jambo lisilofaa na lina khadaa ndani yake na kutolea hoja juu ya madai yao hao kwa kauli ya Ibnu Abbasi (Radhiyallahu Anhu):-

((لَا يَكُوْنُ لَهُ سِمْسَارًا)). رواه البخاري (٢٢٧٤) ومسلم (١٥٢١).

Jawabu yetu juu ya madai haya: Madai yao haya yakiangaliwa kwa uoni wa nje yataonesha yana usahihi lakini yakiangaliwa kwa uoni wa ndani kwa misingi ya elimu ya dini na dalili zake basi panabainika kuwa madai haya yapo mbali na usahihi kwa hoja hizi zifuatazo:-

(a) Kwanza kauli ya Ibnu Abbasi (Radhiyallahu Anhu) ambayo wao wanaitegemea katika madai yao haya si hoja inayokataza udalali bali ni hoja inayoonyesha kuwa udalali ni jambo ambalo lipo na linakubaliwa na sheria ya uislamu kwani kauli ya Ibnu Abbasi imekuja kutafsiri maneno ya Mtume (Salallahu Alayhi Wasallam) pale aliposema:

((وَلَا يَبِيْع حَاضِرُ لِبَادٍ)) رواه البخاري ومسلم .

“ Na wala hauzi mkaazi kwa ajili ya mjaji anaetoka nje ya mji”.

Maana yake: Mjaji anaekuja na bidhaa zake kutoka nje ya mji akija katika mji anatakiwa auze yeye mwenyewe na asiweke dalali amuuzie kwani akiweka dalali akimuuzia atawauzia kwa bei ya juu sanna na akiuza yeye mwenyewe atauza kwa bei ya chini ambayo itawarahisishia watu na kuwaletea manufaa, kwa hiyo katika sura hii haifai kumuweka dalali lakini sura nyengine dalali atafaa kuwepo na ndo maana akasema shekhe Abdul-Muhsin bin Abdillah Azzaamil (Hafidhahullahu) kwa maneno yake haya yafuatayo:-

" دلّ هذا (يعنى قول ابن عباس رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) على أنّ السمسار موجود معروف، لكن في هذه صورة ممنوع ".

“ Imejuulisha hii (yaani kauli ya Ibnu Abbasi) juu ya kuwa dalali ni jambo lilokuwa lipo na linalojulikana na kukubalika lakini katika sura hii ni jambo linalozuilika na kukataliwa”.

Pia kauli ya Ibnu Abbasi iliyotangulia inayosema kama ifuatavyo:-

" لَا بَأْسَ أَنْ يَقُوْلَ: بِعْ هَذَا الثَّوْبَ، فَمَا زَادَ عَلَى كَذَا وَكَذَا فَهُوَ لَكَ ".

“ Hakuna ubaya kusema: Uza nguo hii, na kitakachozidi juu ya kadhaa wakadhaa (Zaidi ya hapo) basi hicho ni chako”.

Kauli hii inaweka wazi zaidi kuwa jambo la udalali ni jambo linalofaa na kauli hii inabatilisha ufahamu mbaya unaopatikana kwa baadhi ya watu katika kauli ya Ibnu Abbasi inayosema:

" لَا يَكُوْنُ لَهُ سِمْسَارًا".

Wakiitegemea kauli hiyo kuliharamisha jambo la udalali na kusema kwao kuwa ni jambo lisilofaa, kusema kwao huko kunahesabika ni ufahamu mbaya ambao unapingwa na kauli yake nyengine Ibnu Abbasi ambayo yeye mwenyewe amehalalisha udalali na kuona hakuna ubaya katika kazi ya udalali.

Basi madai yao hayo yatakuwa yamebatilika na usahihi ni huu ewe muislamu zinduka na fuata dalili na wacha kufuata shubha na ufahamu mbaya wa baadhi ya watu kwani dalili haipo kwenye ufahamu mbaya.

(b) Amma kuhusu khadaa hii ni sifa ya ambayo popote pale itakapopatikana katika jambo basi elewa jambo hilo litakosa barka na mtu akiwa na sifa hiyo basi mtu huyo atakuwa ni katika watu wa motoni kama alivyosema Mtume (Sallahu Alayhi Wasallam):-

((مَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا، والمكرُ، والخداع في النّار)).

“ Yoyote atakaetufanyia khiana si katika sisi, na mwenye kufanya vitimbi na mwenye kufanya khadaa ni watu wa motoni”.

Na ndo maana tukasema mwanzoni mwa kitabu chetu hichi kuwa miongoni mwa sharti ya usahihi wa kazi hii ni kuwa Dalali ajiepushe na khiana jambo ambalo ndani yake khadaa imebebwa kwa hiyo kuwa mtu ana sifa mbaya na akawa na sifa hiyo anaidhihirisha mpaka kwenye kazi yake ambayo kazi hiyo imehalalishwa na sheria ya uislamu, sifa hiyo haiharamishi kazi ambayo iliyohalalishwa na uislamu bali yeye atakuwa ameingiza uharamu kwenye kazi ambayo asili yake ni halali, kwa hiyo madai yao haya yatakuwa yamebatilika.

2- Madai ya baadhi ya watu kusema kwao: “ kuwa udalali wanachuoni ni jambo walilolichukia”.

Jawabu yetu juu ya madai hayo: kwanza; tumeona kauli za wanachuoni wakijuzisha jambo la udalali na kuwa ni jambo la halali na pato litakapopatikana kwa kazi ya udalali kuwa ni pato la halali lisilo na mashaka ndani yake;

Pili: Ni kuwa wanachuoni wamechukia sura ya udalali na siyo kuchukia udalali wenyewe kwani wanafahamu kuwa udalali ni jambo linalokubalika na miongoni mwa sura wanazozichukia ni hizi zifuatazo:

i. Haifai kuwepo dalali kwa mjaji anaetoka nje ya mji kinachotakikana auze yeye mwenyewe bidhaa yake na asiwepo dalali na endapo ataweka dalali hapo ndipo panapatikana chukizo na uharamu katika sura hii kama ilivyokuja katika hadithi.

ii. Haifai kuwepo dalali ambaye hakuna makubaliano baina yake na mmiliki wa mali na endapo atakuwepo dalali ambaye hana makubaliano na kuwafikiana na mmiliki wa mali au mnunuzi wa bidhaa, hapo ndipo pataingia chukizo na uharamu wa udalali.

iii. Udalali katika mali ya haramu au bidhaa ya haramu, hapo udalali haufai na ni haramu kuingia katika jambo la haramu, na zipo baadhi ya sura nyengine pia zikipatikana hizo itakuwa udalali haufai kwa hiyo ni vyema dalali kuifanya kazi hii kwa elimu ili aepukane na makosa.

Na endapo tutajaaliya kuwa wanachuoni wamechukia baadhi yao mas-ala ya udalali basi ni vyema watu wakarudi kwenye dalili na wakashikamana

nazo kwa ufahamu wa wema waliyotangulia na katika mas-ala haya dalili zimekuja na ufahamu wa wema pia umekuja akiwemo Ibnu Abbasi (Radhiyallahu Anhu), kwa hiyo madai yao haya yamebatilika na hayana mashiko yoyote yale.

3- Madai ya tatu: ni kuwa gharama wanazipandisha sana na viwango vyao ni vikubwa sana mpaka panakosekana Imani na madalali, na hivyo tunaona ni kazi isiyofaa. Kwani wao huwakomoa wanunuzi au wauzaji kwa maana wamiliki wa mali.

Jawabu yetu ya madai haya: Mas-ala ya udalali yana sheria zake na utaratibu wake uliyowekwa kisheria kama hadithi iliyokuja kuelezea juu ya masharti wanayokubaliana waislamu:-

((المُسْلِمُوْنَ عَلَى شُرُوْطِهِم))

“ Waislamu wapo juu ya masharti yao ”

Kwa maana waislamu wapo juu ya masharti waliyokubaliana na miongoni mwa masharti ni kufunga mkataba baina ya mmiliki wa mali na dalali, kwa hiyo hata ikionekana dalali ameuza bidhaa kwa gharama ambazo zinaonekana zipo juu huenda ikawa ndo makubaliano yao baina yake na mmiliki wa mali, hili lisipelekee kuitia kwenye uharamu kazi ya udalali pamoja na kuwa dalali anatakiwa asifanye tamaa kwenye kazi yake ya udalali kwa kuuza kwa gharama za juu, bali atakiwa afanye wepesi kwa ndugu zake waislamu na kuwahurumia ili na yeye ahurumiwe na Mola wake Mlezi kama zilivyokuja hadithi katika jambo hili:-

((الرَّاحِمُوْنَ يَرْحَمُهُمُ الرَّحمنُ. ارحَموا مَنْ في الأرض يَرْحَمكُم مَنْ في السماء)) الحديث.

أخرجه أبو داود (٤٩٤١) والترمذي (١٩٢٤) وغيرهما وصححه الألباني في ((صحيح الترمذي)) من حديث عبد الله بن عمرو رضي الله عنه.

“ Wenye kuhurumiana hurehemewa na Allah Mwingi wa Rehma. Wahurumieni wale waliyo katika ardhi atakuhurumieni na kukurehemuni yule aliye kuwa juu”.

Hii hadithi inajuulisha kila kiumbe hadi dalali ambaye huyu akiwafanyia viumbe wa Allah (Subhanahu Wataala) wepesi na kuwahurumia na akawa asifanye tamaa juu ya kazi yake ya udalali, basi atarehemewa na yeye na Mola wake Mlezi na kutiwa baraka ndani yake.

NASAHA MUHIMU KWA MADALALI

Madalali wengi wao ni watu ambao wanaifanya kazi hii ya udalali bila ya elimu, na hili ni kosa mtu kufanya jambo kwa ujinga kwani yoyote anaefanya jambo kwa ujinga basi kukosea kwake ni kukubwa kuliko kupatia kwake na ndio maana ikawa kutafuta elimu ni jambo la lazima kwa kila muislaamu:-

((طَلَبُ العِلْمِ فَرِيْضَةٌ عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ)) الحديث. أخرجه ابن ماجة (٢٢٤) وغيره وصححه الألباني في ((صحيح الجامع)) (٣٩١٤).

“ Kutafuta elimu ni faradhi juu ya kila Muislamu basi ewe dalali uliyekuwa unafanya kazi hii kwa mazoea, badilika na jifunze kazi yako ili ujuwe ni upi uhalali wake na upi uharamu wake ili ufanye jambo ambalo litakalokupa manufaa katika dunia yako na akhera yako.

Lakini pia madalali wengi wana tamaa ya hali ya juu na kuwapandishia wanunuzi zile bidhaa walizokabidhiwa zaidi ya hali ya kawaida ni jambo lilokuwa si zuri basi epukana nalo ewe dalali ili hali yako iwe nzuri, kwani sheria ya uislamu imekataza kupandishiana bei zaidi ya hali ya kawaida:-

((... وَلَا تَنَاجَشُوا ...)) الحديث. رواه البخاري (٢١٥٠) ومسلم (٢٥٦٣) من حديث أبي هريرة رضي الله عنه.

“ … Na wala msipandishiane bei (gharama) …”.

Kwa hiyo; Dalali anatakiwa asiwe na tamaa na akawa ni mwenye kuwakomoa ndugu zake waislamu kwa kuwapandishia bei eti kwa kuwa ameruhusiwa na mwenye mali au mmiliki wa bidhaa husika, haifai kufanya hivyo ewe dalali na chunga uhalali wa kazi yako isijebadilika ikawa ni ya

haramu. Pia dalali ajitahidi kumtegemea Allah (Subhanahu Wataala) katika kazi yake hii ya udalali kwani wengi wa madalali hufanya ushirikina katika kazi yao ya udalali na ushirikina huo huufanya kwa lengo la kuwavutia wateja ili wainunue bidhaa, kufanya kwao huku ni kumkera Mola wao mlezi aliyewaumba, haifai kufanya shirki bali mtegemee Allah atakupa kile unachokitaka kwa kumuomba yeye na kumuabudu na kumukhofu yeye peke yake:-

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجٗا ۝٢ وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ حَيۡثُ لَا يَحۡتَسِبُۚ وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓۚ إِنَّ ٱللَّهَ بَٰلِغُ أَمۡرِهِۦۚ قَدۡ جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُلِّ شَيۡءٖ قَدۡرٗا ۝٣﴾ [الطَّلَاق : ٢ - ٣]

“ Na yoyote mwenye kumcha na kumuogopa Allah humtengenezea njia ya kutokea. Na humruzuku kwa namna asiyotazamia wala kuitarajia, na anayemtegemea Allah basi yeye Allah humtosha, hakika Allah hufikisha mbali jambo lake na kulitimiza. Allah hakika amejaaliya kila kitu na kipimo chake”.

Kwa hiyo ewe muislamu unaefanya kazi hii ya udalali epukana na ushirikina na mtegemee Allah katika hali zako zote kwani ndiko kuna mafanikio yako na shirki haina manufaa isipokuwa ni kuangamia duniani na akhera, basi zinduka ewe dalali juu ya hili usikubali kuuza dunia yako kwa akhera yako.

Jambo jengine la kumnasihi dalali ni kuwa subra ni jambo muhimu na jambo la subra siyo kwenye udalali tu bali ni katika kila jambo ni vyema muislamu ili afanikiwe ashikamane na subra na ndo maana mwenye kusubiri hulipwa malipo yake bila hesabu:-

﴿إِنَّمَا يُوَفَّى ٱلصَّٰبِرُونَ أَجۡرَهُم بِغَيۡرِ حِسَابٖ ۝١٠﴾ [الزُّمَر : ١٠]

“ Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hesabu”.

Kila anaefanya la kheri ambalo linazingatiwa na sheria ya uislamu na akawa anakutana na mambo ambayo yanahitaji kufanya subra ndani yake basi ni juu yake kujilazimisha na subra kwani ndiko kunako mafanikio na hata wewe dalali unaefanya kazi ya udalali kwa misingi sahihi ya uislamu ni juu yako kushikamana na subra na kutokukata tamaa na rehma za Mola wako mlezi:-

﴿لَا تَقۡنَطُواْ مِن رَّحۡمَةِ ٱللَّهِ﴾ [الزُّمَر : ٥٣]

“ Wala msikate tamaa na rehma za Allah”.

Jambo la kukata tamaa ni jambo la sheitani na jambo la subra ni jambo la Allah (Subhanahu Wataala) na ndo maana Allah akasema yupo pamoja na wenye kusubiri.

﴿إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٥٣﴾ [البَقَرَة : ١٥٣]

“ Hakika Allah yupo pamoja na wenye subira ”.

Kwa hiyo ewe dalali ukilifahamu hili utakuwa ni mwenye kushikamana nalo.

NASAHA ZINAZOFUNGAMANA NA UTEKELEZAJI WA AHADI NA MIKATABA KWA MADALALI, WAMILIKI WA MALI NA WANUNUZI WA MALI HIYO AU BIDHAA

Wamiliki wengi wa mali wanapofunga mikataba ya miamala ya kibiashara huwa wanaitengua mwisho wake kwa kipato ambacho kinachoingia baada ya mauziano kukamilika, huwachukua tamaa ya kuwafanya watengue mikataba hiyo, jambo ambalo lipo kinyume na sheria ya uislamu kwani uislamu umehimiza kuitekeleza ahadi na mikataba inayofungwa na kuepuka kutengua ahadi hizo na mikataba hiyo:-

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَوۡفُواْ بِٱلۡعُقُودِ﴾ [المَائِدَة : ١]

“ Enyi mliyo amini: Timizeni ahadi”

Hii ni aya inayohimiza kutekeleza ahadi na kuzitimiza, ikiwa mtu ameweka ahadi kwa mfanyakazi wake kuwa atamlipa kiwango maalumu cha mshahara kisha akatengua ahadi hiyo na mkataba huo, basi ajue kuwa amefanya jambo ambalo la kumuasi Allah na kuziasi amri zake, na yoyote mwenye kuasi amri za Allah huyu ataingia motoni, kwa hiyo ewe dalali na ewe mmiliki wa mali na wote waliyofunga mikataba ni juu yenu kuchunga ahadi zenu pamoja na mikataba muliyoifunga ili muepukane na adhabu za Allah (Subhanahu Wataala), na pia kutengua ahadi ni katika alama za watu

wanafiki wanapoahidi hawatekelezi kama zilivyokuja hadithi kuelezea watu wa aina hiyo.

Dalali hawi mzuri katika kazi yake mpaka pale atakapoacha kutengua ahadi na akawa mbali na sifa hii mbaya na vile vile mmiliki wa mali au bidhaa hatokuwa mzuri katika hali zake mpaka pale atakapokamilisha ahadi zake na kuzitimiza.

DALALI WAPI ATACHUKUWA UJIRA WAKE JE ATACHUKUWA KUTOKA KWA MMILIKI WA MALI AU KWA MNUNUZI AU KITAKACHOZIDI NDICHO ATAKACHOCHUKUWA

Mas-ala haya ya dalali kuwa wapi atachukuwa ujira wake ni mas-ala muhimu pia kufahamika kwa mujibu wa dalili zilizokuja na kauli za wanachuoni juu ya mas-ala haya, panabainika haya yafuatayo:-

a) Dalali atakapokubaliana na mmiliki wa mali kuwa achukue kitakachozidi baada ya kuuzwa kwa mali au bidhaa basi atachukuwa hicho kilichozidi.

b) Dalali atakapokubaliana na mmiliki wa mali au bidhaa kuwa atapewa kiwango maalumu atakapouza bidhaa ya mmiliki basi ujira wake utakuwa ni huo aliyokubaliana na mmiliki kuwa atampa kiwango hicho.

c) Wakati mwengine dalali huambiwa na mnunuzi kuwa nitafutie bidhaa fulani na nitakupa kiwango fulani na wakakubaliana juu ya kiwango hicho basi hapo ndipo ulipo ujira wa dalali.

d) Na pia dalali wakati mwengine hufunga makubaliano kwa muuzaji kwa kumtafutia mteja atakaenunua bidhaa yake na wakati huo huo amekubaliana na mnunuzi pia atapewa kiwango maalumu kwa hiyo huchukuwa kutoka pande zote mbili, basi hakuna ubaya kufanya hivyo na ndo maana wanachuoni wakasema haya yafuatayo:-

" وأمّا أخذ السمسار أجرة من البائع والمشتري فلا بأس به إذا كان مشروطًا أو جرى العرف بذلك".

“ Na amma kuchukuwa kwa dalali ujira kutoka kwa muuzaji na mnunuzi, basi hakuna ubaya itakapokuwa jambo hilo limewekewa sharti au pamepita urfu (desturi) za watu katika jambo hilo”.

TANBIHI: Desturi za watu zinazingatiwa ndani ya sheria ya Uislamu itapokuwa desturi hizo hazipingani na Uislamu na endapo zitapingana na uislamu basi desturi hizo zitaachwa na kupingwa na kukutazwa.

KUZIWEKA SAWA DHANA ZA WALE WENYE FIKRA POTOFU JUU YA KAZI YA UDALALI

Kama ilivyokwisha tangulia kubainishwa dalili zinazoonesha kuwa kazi ya udalali ni kazi inayofaa kisheria pale itakapotimiza sharti zinazotakikana katika kazi hiyo:-

Kwa kujengea maelezo hayo, kuna baadhi ya watu wana dhana potofu juu ya kazi hii ya udalali na kuona ni kazi mbaya tena ni ya haramu na kuwasema vibaya madalali kwa kazi yao hii !!!

Dhana zao hizi zimejengeka kwa wengi wao kutokana na ukosefu wa elimu inayohusiana na udalali ndio maana ikawapelekea waone kuwa kazi hii ni kazi ambayo haifai na ni mbaya, hizi dhana ambazo walizoziweka au zilizojengwa ndani ya nyoyo zao ni dhana zilizokuwa mbali na dalili na dhana haisaidii chochote kwenye haki kama Allah (Subhanahu Wataala) alivyosema:-

﴿وَمَا لَهُم بِهِۦ مِنْ عِلْمٍۖ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّۖ وَإِنَّ ٱلظَّنَّ لَا يُغْنِى مِنَ ٱلْحَقِّ شَيْـًٔا﴾ [النَّجم : ٢٨]

“ Na hawana ujuzi wowote kwa hayo, isipokuwa wanafuata dhana tu. Na dhana haisaidii chochote mbele ya haki”.

Upeo wa watu hawa wanaodhania kuwa kazi ya udalali ni kazi iliyokuwa mbaya sana tena ni kazi ya haramu ni kule kuyahesabu yale yanayofanywa na baadhi ya madalali waliyokuwa hawana elimu ya hii kazi na wakawa wanaifanya kwa uzoefu tu pasi na elimu, kwa hiyo wao wakatolea hukmu ya kuwa kazi ya udalali haifai kwa yale yanayofanywa na baadhi ya madalali.

Haki inajulikana kwa dalili na siyo kwa vitendo vya watu na huu ni msingi muhimu kwenye mas-ala ya dini yetu ya uislamu, kama walivyosema wanachuoni:-

" اعرف الحق تعرف أهله، وإنما يعرف الحق بالأدلة ولا يعرف الحق بالرجل ".

“ Itambue (kwanza) haki, utawatambua watu wake (watu wa haki), na hakika hujulikana haki kwa dalili na wala haijulikani haki kwa watu wala kwa vitendo vya watu”.

Kwa maneno haya ya wanachuoni, inabainika upotovu wa dhana za watu wanaodhania kuwa kazi ya udalali ni kazi isiyofaa na hali ya kuwa dalili zimekuja juu ya kufaa na kuhalalika kazi hii.

ANGALIZO: Tabia na vitendo vya baadhi ya madalali ni kweli ni vibaya sana kwa sababu ya ukosefu wa elimu inayofungamana na mas-ala ya udalali, kwa hiyo ewe dalali kabla ya kuiingia kazi hii basi ni vyema kuijua elimu yake ili kuepuka kufanya jambo kwa ujinga.

" العلم نور والجهل ظلام".

“ Elimu ni nuru na ujinga ni giza”.

Elimu itakuangaza kwenye kazi yako ya udalali endapo utakuwa ni mwenye kuwa na elimu ya udalali kwa misingi ya uislamu na ujinga ni giza linalopoteza na kuharibikiwa ndani yake.

HITIMISHO

Mwisho kabisa tunamshukuru Allah (Subhanahu Wataala) kwa kutupa taufiq ya kukiandika kitabu hiki ikiwa tunakusudia kuwaekea muangaza wa elimu wale wote wanaojishughulisha na kazi ya udalali kwani wengi wao hawaifanyi kazi hii kwa elimu. Tunamuomba Allah (Jalla Jalaaluhu) kwa majina yake matukufu na sifa zake kamilifu aifanye kazi hii iwe na ikhlasi na iwe ni yenye kuwanufaisha waja wote na uislamu kwa ujumla wake.

(Aaamin)

KIMETAYARISHWA NA KUANDIKWA NA

ABUU MUHAMMAD HASNUU AMOUR KOMBO

AZZINJIBARIY ATTANZANIY

MAKTABATUL IMAMIL AUZAAI'Y
ZANZIBAR TANZANIA
0779819880 0772719464
0776959197